Hapo, sina ubishi. Lakini sasa tunampa madaraka huyu kamishna, ambaye ni mtu binafsi, na siyo kamati, ili afanye vile anataka. Anaweza kufanya vile atakavyo, kulingana na ile Harambee atatoa. Mimi sichukii Harambee lakini maovu mengi yanafanywa katika jina la Harambee. Siku hizi, ikiwa wewe hauna pesa, wewe si mtu. Hawajali akili yako ila kile kilicho katika mfuko wako. Hata kama umemua mtu na umemnyang'anya pesa zako upeleke kwa Harambee Bunyore kwa mhe. Muchilwa, utapata makofi ya kilo. Hawana haja ya kuuliza ulipata wapi hizo pesa. Utapewa tu makofi ya kilo. Hata Harambee zikifanywa, hakuna kitu kinajengwa. Hakuna hata nyumba moja hujengwa. Pesa hizo zinaliwa tena na wakubwa wengine wa sehemu hiyo.

Zangu Kshs1.8 milioni zilizokusanywa zililiwa. Mtukufu Rais alisema mshahara wake na kila kitu cha Butere kigawanywe. Hakuna kitu hata kimoja kilijengwa. Pesa zimeliwa. Ni kwa nini tunampa huyu kamishina ambaye ni mtu mmoja binafsi hizi nguvu zote?

Mr. Nthenge: Jambo la nidhamu, Bw. Naibu Spika wa Muda. Ni nidhamu kwa mhe. Shikuku kusema kwamba pesa zake zaidi ya milioni moja zilizowekwa kwa maendeleo ya Butere zililiwa? Anaweza kuondoa dai hilo au atuonyeshe vile pesa hizo zilivyoliwa?

Mr. Shikuku: Bw. Naibu Spika wa Muda, mhe. Nthenge anatafuta matata kwangu na atayapata. Mimi ninavyosema katika Bunge hili huwa na ushahidi. Katika mwaka wa 1968, nilileta Hoja katika Bunge hili kusema kwamba, wakubwa wakatwe mishahara, 15, kumi, tano na moja, ili ziweze kusaidia watu wasiokuwa na kazi, kwa kuanzisha viwanda vidogo.

The Temporary Deputy Speaker (Mr. Wetangula): Mhe. Shikuku, unatakiwa kuthibitisha ya kwamba pesa zako zaidi ya milioni moja zililiwa. Ni hiyo tu!

Mr. Shikuku: Ninamweleza vile nilipata hizo Kshs 1.8 milioni.

The Temporary Deputy Speaker (Mr. Wetangula): Hapana. Hakuuliza vile ulizipata. Anataka uthibitisho vile zililiwa.

Mr. Shikuku: Bw. Naibu Spika wa Muda, zilitolewa kutoka Kenya Commercial Bank tawi la Mumias na kuliwa. Mshahara wangu ulikuwa ukikatwa na kwenda huko. Pesa zangu na za watu wa Butere zilikuwa ndani, na zikatolewa na Mkuu wa Mkoa wakati huo, Bw. Kobia, na hakuwa mweka sahihi huko Butere. Alisema amri imetoka juu. Ng'o! Pesa zikatolewa na mpaka leo, hakuna hata mradi mmoja huko Butere uliojengwa na hizo Kshs1.8 milioni. Zimeliwa! Mimi nangojea mtu mmoja atakapowacha kazi, nimpelike kotini. Na ni yule aliyesema zitolewe. Hivi sasa, sheria inasema siwezi kumpeleka kotini. Kwa hivyo---

An hon. Member: Alikufa!

Mr. Shikuku: Hapana! Hajakufa na bado yuko. Aliyekufa ni Bw. Kobia na ni yeye alitoa. Lakini aliyemtuma ndiye nataka kumushtaki. Haiwezekani kwa sasa kwa sababu haiwezekani sasa. Nangojea mpaka siku ile atatoka ili nimshtaki.

Mr. Nthenge: Na akifa!

Mr. Shikuku: Shauri yake! Nitampata kule mbinguni.

Bw. Naibu Spika wa Muda, kumpa madaraka haya yote mtu mmoja si vizuri. Nafikiri Waziri atalichunguza jambo hili ili madaraka yapewe kamati ya watu wengi kufanya kazi hiyo. Siyo mtu mmoja.

Pia, ukiangalia katika ukurasa wa 133, kuna Cap. 489 na kumeandikwa:

(ii) A building society registered under the Building Societies Act, which in the case of housing bonds, has been approved by the Minister for the purposes of this Act, or

(iii) The Central Bank of Kenya:

Provided that in the case of housing bonds, the aggregate amount of interests shall not exceed Kshs300,000, and--

Bw. Naibu Spika wa Muda, Waziri hapa ana madaraka ya kuidhinisha shirika lolote lile la ujenzi. Hakuna sehemu hapa ambayo inaonyesha kutakuwa na ukataji wa rufani. Madaraka yake ni kuidhinisha tu, na hakuna kamati ya kuangalia hayo maneno. Ni yeye tu.

Katika marekebisho ya Mswada wa Fedha, ningelipenda kuzungumzia jambo moja, lakini mhe. Muite tayari amefanya hivyo. Nitaliwacha hivyo hivyo.

An hon. Member: Rudia ili usisitize!

Mr. Shikuku: Watasema navunja Standing Order No. 87.

Kwa hivyo, Bw. Naibu Spika wa Muda, ningependa kusema kwamba wakati Hoja hii itakapoingia katika Kamati, kuna vifungu vingine hapa ambazo ningehitaji kuelimishwa zaidi kwa nini zimeletwa hapa. Wakati huo ukifika, ndio nitoa maoni yangu kulingana na mabadiliko haya kwa sababu ukiangalia katika Hoja hii na uilinganishe na mabadiliko haya, utapata kuwa kuna mahali pengine ambapo mabadiliko haya yamefanywa vizuri hapa katika Order Paper kuliko katika Hoja hii. Wakati huo ukifika, nitaweza kutoa maoni yangu.

Lakini hivi sasa, nitamaliza ili niwape Wabunge wengine fursa ambao wanataka kuzungumza, wazungumze. Ikiwa Serikali hii haiweze kuacha mwenendo ulioko sasa ambao watu hutoa kodi na hawaoni faida yake, ni mwenendo mbaya. Kwa sababu mwenendo huu ulileta madhara kule Uingereza. Mfalme alikuwa anapata fedha kutoka kwa watu naye alikuwa anazitumia vile anavyotaka na kujali. Iibidi watu wakati mmoja kusema kwamba "hatuwezi kutoa kodi mpaka maoni yetu yatakaposikilizwa". Kuna mmoja aliyekazania wito huo mpaka akakatwa shingo. Sisi tuko hapa katika Bunge hili. Waingereza walisema kuwa "No taxation without representation". Nasi pia hapa tunatoa kodi, lakini hatupati huduma kutoka kwa kodi hiyo. Bado tunasema kuwa Serikali hii lazima iwape watu huduma zinazohitajika, lakini haitoi huduma hizo ingawa wanachukua kodi. Wakati utafika ambapo tutasema kuwa hatutoi kodi mpaka tuone huduma zetu. Kwa sababu sisi Wabunge ndio tunapewa taabu sana na wananchi kwa kuulizwa hili na lile, lakini sisi katika Bunge hili tunahalalisha Hoja hii na baadaye tutapitisha Appropriation Bill na pesa zinakwenda kwa Serikali, Serikali inavuja pesa, lakini tukifika katika majimbo yetu ya uwakilishi Bungeni, tunapata taabu kutoka kwa wananchi. Hawana habari kuwa ni Serikali imevuja pesa zao. Ninataka wananchi waelewe kuwa kazi ya Mbunge ni kupitisha fedha katika Bunge hili na wala hapakulii chakula watu wake. Kuna wale ambao wanapakua na wanaitwa watumishi wa Serikali.

Ukitaka kuona watu walio matajiri, utapata kwamba matajiri wote walikuwa watumishi wa Serikali kwa wakati fulani katika maisha yao. Hata ikiwa ni Mbunge, alikuwa mtumishi wa Serikali na ukichunguza sana utagundua kwamba mali yake aliyapata kutoka umma. Huu ndio ukweli mtupu. Kwa hivyo, wananchi wasije wakawa wanababaisha Wabunge wao. Mbunge akishafika hapa na kupiga kura ya kutoa fedha hizi na kutoa maoni yake juu ya shida za watu wake, kazi ya Mbunge imekwishia hapo. Ikiwa hakuna maendeleo, mtu ambaye anatakiwa kuulizwa ni Mkuu wa Wilaya na Serikali kwa sababu Mkuu wa Wilaya ndiye mwenyekiti wa DDC na fedha zikitoka hapa, zinaenda kwake, si kwa Mbunge. Kwa hivyo, hakuna haja kwa wananchi kujua kusumbua Mbunge kwa kumwuliza eti amefanya nini. Atafanya nini naye amekwisha piga kura yake na pesa zimekuja na kuvujwa huko katika Wilaya? Hata katika PAC, watu ambao wamenyanyasa watu na kuvuja pesa za umma ni wale watumishi wa Serikali katika Wilaya. Kwa kufanya hivyo, wanaua Waafrika wenzao kwa sababu wakitoa huduma zao kwa Serikali, hawalipwi. There is what we called Pending Bills. Wanaua wale Waafrika wenzao wanaojaribu kusimama kifedha kwa kutowalipa kwa huduma wanazotoa kwa Serikali. Hii ndiyo sababu kuna shida hii ya Pending Bills mwaka baada ya mwaka. Serikali hii ni mbovu sana.

Kwa hayo machache, Bw. Naibu Spika wa Muda, ninaunga mkono.

The Assistant Minister for Information and Broadcasting (Mr. Nassir): Bw. Naibu Spika wa Muda,

ninakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Pia ninamshukuru mwenzangu, mhe. Shikuku, kwa sababu baada ya yote aliyoyasema, mwisho anakubali tutoze watu kodi ili tuweze kuendesha Serikali yetu.

Bw. Naibu Spika wa Muda, tutakuwa na taabu kila Kenya inapoendelea kwa sababu bajeti tunazozifanya watu wengi na makadirio ni machache. Ukimwuliza mwenzako kuna watu wangapi Kenya, mmoja atakwambia ni 25 million, mwingine atasema 30 million na mwingine atakwambia 36 million. Lakini kwa sababu ya starehe na amani iliyoko hapa nchini, nchi haina njaa, tunastarehe kweli kweli na tunazaa. Ninaomba Mungu atujalie tuzae zaidi kwa sababu hakuna ubaya kuzaa.

Bw. Naibu Spika wa Muda, mimi na wenzangu wengine hii si Serikali ya kwanza ambayo tumeona, tulitoka kutoka Serikali ya Sultan, Serikali ya Mwingereza, Serikali ya hayati Mzee Kenyatta na Serikali ya Moi.

Mr. Orenge: Wewe umekuwa katika vyama vingapi?

The Assistant Minister for Information and Broadcasting (Mr. Nassir): Bw. Naibu Spika wa Muda, mhe. Orenge ananiuliza habari za vyama, lakini nilikuwa na chama cha kuogofya watu kama mhe. Orenge wa kutumaliza sisi watu wachache. Tulikuwa na vyama vingi, lakini chama ambacho tulikuwa tunaogopa kati ya vyama hivi ndicho hiki kinakuja sasa cha kuunganisha makabila makubwa kutaka kuyanyonga makabila madogo.

Bw. Naibu Spika wa Muda, mambo yanaenda yakilegea. Ikiwa mwendo ni huu wendao, asifikirie kuwa kutatokea mengine. Lakini ninataka kusema kuwa kati ya Serikali zote nilizoziona, mimi na wenzangu tuliokuwako kama mhe. Shikuku, tuliona ubaguzi wa rangi, kuandikisha kazi, utoaji wa mashamba na leo kama mtu si binadamu ambaye anashukuru Mungu, hawawezi kushukuru. Yale yalioko sasa ni kila Mkenya leo, hata mimi na ubaya na mvi zangu, ninajivuna nenda. Wakati ule ambao tuliona, mhe. Orenge alikuwa mtoto mdogo akitoka shule na visuali vya kipande, ulikuwa unaambiwa ukisema zaidi hata mhe. Shikuku, aliambiwa utalionia chui likija kukuchukua. Aliambiwa, "tena fanyieni adhabu zenu". Lakini leo tunashukuru Mungu kwa sababu tuna watu ambao wanaweza kusema watakalo. Hii ndiyo demokrasia ambayo tunataka ingawa wengine hawaitaki.

Bw. Naibu Spika wa Muda, nchi nyingine jirani hazina vyakula, pahali pa kulala, kazi, wanakufa njia na hawana dawa, lakini---

Mr. Shikuku: Jambo la nidhamu, Bw. Naibu Spika wa Muda. Mhe. Mbunge anasema kuwa sasa tuna Uhuru wa kusema, lakini tulikuwa na Uhuru wakati wa Kenyatta na nilikuwa ninazungumza katika Bunge hili. Lakini ninataka kujua mhe. Mbunge anazungumzia juu ya sehemu gani ya Mswada huu? Mhe. Keah amenyamaza kimya, haulizi.

The Assistant Minister for Information and Broadcasting (Mr. Nassir): Ninakubali, Bw. Naibu Spika wa Muda. Lakini ikiwa ni kushindana kuzungumza, mhe. Shikuku alisema kuwa alichaguliwa na watu wa Butere ili aje azungumze hapa. Mimi nilichaguliwa ili nifanye kazi kwa kusaidiana na wenzangu kuwatafutia kazi. Na ikiwa mtu ni mgonjwa nimepeleke hospitali. Mimi nimechaguliwa namna hiyo. Lakini yeye anasema kuwa mtu asimwendee nyumbani kwake baada ya kumchagua kumwomba msaada kwa sababu kazi yake ni kuja kuzungumza hapa. Siamini kama kazi yangu ni kuja kuzungumza hapa. Mimi ni mtumishi wa umma na niko tayari kuwatumikia wananchi.

Bw. Naibu Spika wa Muda, hata kuna viongozi wengine ambao wamekataa kufanya Harambee hapa nchini na idadi ya watu ilivyo wakati huu ni kubwa sana na Serikali hii ambayo haina dhahabu wala mafuta haiwezi kuwafanyia watu miradi yote ya kimaendeleo. Nastaajabu mhe. Shikuku kusema hakuna haja ya kufanya Harambee kwa sababu viongozi wetu ni wezi. Wenzake aliyonao katika chama kimoja cha kisiasa wanafanya Harambee na kupeleka watu wao ulaya na wanafanya biashara na yeye anakazanakazana na kusema maneno matupu---

Mr. Shikuku: Nasimama kwa jambo la nidhamu, Bw. Naibu Spika wa Muda. Ni haki kwa mhe. Nassir kunizingizia maneno ambayo sikuyasema? Ninasema tunatoa kodi kwa Serikali na ni wajibu wa Serikali kufanya yale wananchi wanayohitaji wala si Wabunge. Yeye anasema habari ya Harambee, je, anaweza kutuonyesha anazingatia kifungu kipi katika Mswada huu? Nilipokuwa nikuzungumza mhe. Keah hangenipa nafasi ya kuongea bila ya mimi kuzingatia Mswada huu na wakati huu mhe. Keah amekaa kimya tu haulizi chochote. Ni kifungu gani katika Mswada huu ambacho mhe. Nassir anazungumzia juu yake?

The Assistant Minister for Information and Broadcasting (Mr. Nassir): Bw. Naibu Spika wa Muda, Mswada huu unajishughulisha na kila jambo. Ni lazima tuzungumze juu ya huo Mswada. Mhe. Keah ni Waziri Msaidizi wa Fedha na mimi ni mhe. Nassir, nasema yangu wala si ya mhe. Keah---

Mr. Shikuku: Nasimama kwa jambo la nidhamu, Bw. Naibu Spika wa Muda. Hata mhe. Nassir hana nakala ya Msadwa huu, je ni haki yeye kuzungumza juu ya jambo lolote bila kuzingatia Mswada huu? Mhe. Shikuku akizungumza lolote bila kuzingatia Mswada huu anaulizwa na mhe. Keah ambaye wakati huu amekaa

kimia na hamuulizi mhe. Nassir ni kifungu gani katika Mswada huo ambacho kinazungumza juu ya Harambee.

The Temporary Deputy Speaker (Mr. Wetangula): Mhe. Nassir, zungumza juu ya ushuru.

The Assistant Minister for Information and Broadcasting (Mr. Nassir): Bw. Naibu Spika wa Muda, ninazungumza juu ya ushuru kwa sababu ushuru katika Mswada huu umeguzia mambo yote kwa mapana na marefu. Kama vile vyakula, kusomesha watoto, pesa, jinsi Serikali inavyoendesha shughuli zake na kadhalika.

Bw. Naibu Spika wa Muda, nilikuwa nataka kuwafahamisha wakenya hasa vijana kama mhe. Orenge aliyetoka shule juzi akaenda chuo kikuu na wengine kama vile wanasheria, watu walipata taabu ili tuweze kupeleka Kenya yetu mbele.

Kwa hivyo, Miswada kama hii ikija ni wajibu kujadiliana na ikiwa ni pesa tunatoza zinatumiwa na wakati mwingine tunafanya Harambee. Kuna Wabunge wengine hata kama tukiwa na "Serikali ya dhahabu" watakuwa waitukana tu. Ni tabia yao tu ambayo ni kama ngozi yao. Kama mtu tabia yake ni kukejeli, atakejeli tu hata akiona jiwe atakejeli. Tumekuwa na Serikali siku zote na kila Serikali inaambiwa haya haifanyi sawasawa na kadhalika. Je, mnataka tuilete Serikali kutoka mbinguni ili iwe sawasawa? Si watu ni hawa hawa? Hata mtoto yangu mhe. Nyagah yuko hapo anajua kutoka zama za babake tukifanya kazi hapa kuwatumikia watu si kama leo tunasema maneno tu bila vitendo.

Bw. Naibu Spika wa Muda, katika Kenya kuna demokrasia, mapenzi, amani na kila kitu. Tumefikia hata wakati ambapo wabunge wanasema ya kwamba watawasawishi watu ili wawe na "single presidential candidate." Ikiwa mtoto wako uliyemzaa hawezi kumwambia utaolewa na fulani na fulani, je, itawezekana kumwambia mtu ampigie kura mtu fulani?

Mr. Shikuku: Ninasimama kwa jambo la nidhamu, Bw. Naibu Spika wa Muda. Ningependa sheria zisingatiwe na kila Mbunge katika Bunge hili. Mhe. Nassir anazungumza juu ya "single presidential candidate" na kadhalika. Je, unaweza kumpa mhe. Nassir huo Mswada wako ili atwambie ni kifungu gani cha Mswada ambacho kinazungumza juu ya "single presidential candidate?"

The Assistant Minister for Information and Broadcasting (Mr. Nassir): Bw. Naibu Spika wa Muda nimekuwa mtaalamu kama mhe. Shikuku---

The Temporary Deputy Speaker (Mr. Wetangula): Hon. Nassir, which page are you referring to?

The Assistant Minister for Information and Broadcasting (Mr. Nassir): Bw. Naibu Spika wa Muda, kila ukurasa katika Mswada huu unawahusu Wakenya na maisha yao. Ni kurasa zote ambazo zina mambo ambayo yanawahusu Wakenya.

An hon. Member: Ukurasa gani?

The Assistant Minister for Information and Broadcasting (Mr. Nassir): Bw. Naibu Spika wa Muda, Mswada huu unahusu ushuru au pesa. Hizi pesa zinatozwa watu wa Kenya na ni lazima Wakenya wapate haki zao.

Ninasema kama rafiki yangu, ukweli ni lazima tuseme ukweli na asemaye kesho ni mwongo. Ya leo yawe ya kweli. Ukweli hasa ni kwamba Serikali hii jinsi inavyofanya kazi na jinsi tunavyoina nzuri sana pengine ya Mungu ni mengi watoto wetu watakuja kuona wakija kushikilia madaraka. Watu wengi hawajui lakini mhe. Shikuku anajua wakishika madaraka tutakuwa na hali gani.

Hivi sasa katika Mashariki na Kati ya Afrika, ninaona fahari kuwa hapa nchini Kenya tuna raha na amani. Tunacheza na kufurahika na hata siasa zetu ni nzuri, tunaishi kwa amani. Ndio nikasema Mswada kama huu, mtu anaweza kusema apendalo lakini wale waliona kutoka Serikali ya Sultan, Mwingereza, Hayati Kenyatta mpaka ya leo ni lazima tuseme ukweli. Na mtu kama amekasirika sana atafute vigae na atia ndani ya chupu na anywe!

Bw. Naibu Spika wa Muda, leo tunastarehe Kenya, tuna furaha, chakula na kadhalika na wenzetu jirani wanajaa na hawana madawa. Sisi hapa tuna furaha na watoto wanasoma---

Mr. Shikuku: Ninasima kwa jambo la nidhamu, Bw. Naibu Spika wa Muda. Mhe. Nassir anasema tuna dawa na hali wewe na mimi hatuna dawa na kodi tumetozwa hata kule Mombasa Coast Hospital hakuna dawa, je, ana haki ya kupotosha Bunge hili?

The Assistant Minister for Information and Broadcasting (Mr. Nassir): Bw. Naibu Spika wa Muda, kama nilivyosema labda atoke malaika aje atengeneze Serikali. Bidii tunayo ya kuendesha Serikali iwapokuwa watu ni wengi na Wabunge wezangu hawawezi kuifanya Serikali hii kuwa kama Saudi Arabia, Marekani, Afrika Kusini ambako kuna iron ore na madini mengine. Sisi ni masikini, tuna kahawa, chai, sukari na kadhalika, lakini watu wengine wanaishi katika maisha ya umaskini kabisa. Tumshukuruni Mungu kwa vile kila mkenya anaweza kuamkia kikombe cha chai. Lakini mahali pengine ulimwenguni watu wakufa njaa. Kwa sababu ya starehe tulizo nazo, kwa sababu ya baraka za Mungu tulizo nazo binadamu ni vile vile vidole vitano hatosheki. Hata kama mtu angepewa dhahabu au madini mengine hawawezi kutosheka. Tunawashukuru Wakenya kwa

sababu wanastahimili na wanajua taabu zao. Kitu kikubwa ambacho ninataka kuwaambia wenzangu Wabunge na wale walioko nje ya Bunge hili ni kuwa Serikali ni ya Wakenya. Hii ni Jamhuri ya Kenya, usimtishe mtu ukamwambia kuna Serikali ifanyayo hivi na vile.

Serikali ni hii katika Bunge: Ulipitishalo ndilo liendalo, na haliendi kinyume na hii. Katika hii desturi ya kutoka zamani ya kuwambia watoto wasitoke nje kwa sababu kuna simba mkali au mbwa mkali---

The Assistant Minister for Finance (Mr. Keah): Jambo la nidhamu, Bw. Naibu Spika wa Muda. Nidhamu yangu leo itakuwa tu ni ya kujaribu kupendekeza kwamba tusingize nidhamu zaidi ili tuweze kumaliza na Mswada ambao tuko nao. Ningekuomba tu utusaidie Bw. Naibu Spika wa Muda, hata ikiwa ni Mhe. Shikuku au Waziri Msaidizi, Bw. Nassir ambaye anaongea. Lakini kwa vile sisi katika Wizara tunahitaji usaidizi, watuelekeze kama Mswada huu ni sawa. Ninaomba kupitia kwako kwamba watakaozungumza wajaribu kutueleza katika Mswada huu na Clauses zake ikiwa yawezekana kuliko kuzungumza mengi mazuri; ni mazuri wanayozungumza na mimi ziyakatai lakini kuna wakati wake. Wakati huu ni wakati wa Mswada huu. Na ningeuomba kwamba tujaribu kuwa ndani ya Mswada huu.

The Temporary Deputy Speaker (Mr. Wetangula): Bw. Nassir, tunataka mwelekezo na mwongozo katika mazungumzo yako.

The Assistant Minister for Information and Broadcasting (Mr. Nassir): Bw. Naibu Spika wa Muda, nitawafanyaje wenzangu waupitishie huu Mswada? Kama Naibu wa Waziri ana haraka sijui. Lakini kama hana haraka, aaje awaeleze wenzangu ili tupitishie huu Mswada. Kama ulivyosikia wenzetu jinsi walivyoiponda na kama mimi sikujibu na kukuelekeza upewe pesa haraka, itakuwa taabu. Kwa hivyo, yangu ni kutaka watu wasikisane. Kusema, "wajua hiyo ni Serikali, wajua huyo nani" na wewe mwenyewe ulichaguliwa ili uunde Serikali, ama uje utoe maneno katika Serikali ili kupelekea mambo wayatakayo watu wako.

Kwa hivyo, Bw. Naibu Spika wa Muda, yangu ni kushukuru sisi tunaoendeza nchi na demokrasia yetu. Lakini ningewaomba tu ndugu zangu kwa ruhusa yako wasilazimishe watu kuchagua wawatakao. Hata mtoto msichana wako nyumbani huwezi kumwambia nenda kaolewe na fulani, wacha kupiga kura.

Kwa hayo machache, naunga mkono.

Mr. Maore: Thank you, Mr. Temporary Deputy Speaker, Sir, for giving me this opportunity to say a few words about the Appropriation Bill.

The Temporary Deputy Speaker (Mr. Wetangula) We are going to be very strict on the rule because of relevance. I have been very lenient with hon. Shikuku and Nassir.

Mr. Maore: Mr. Temporary Deputy Speaker, Sir, I would just want to carry on from where hon. Nassir has concluded on the issue of democracy. We need it to deliberate on a Bill in this Parliament since the Government is intact. One cannot do this in Somalia today. That is why it is very relevant and we would wish the Assistant Minister for Finance would be able to find how to squeeze the topic.

Mr. Temporary Deputy Speaker, Sir, the topic of democracy and good governance have been persistently with us for the last five years especially after the fall of communism. The most fortunate issue is that we are dealing with a Government which is being led by a distinguished Kenyan who has had the opportunity to serve the country for 18 years at number one slot, 12 years as number two, which means 30 years. That is my entire life. Now, if as a good Kenyan, you are not grateful for being at the top for 30 years, then the country and Africa is poorer. We do not want to wait for a crisis for KANU to realise that we need a constitutional reform in key areas to make the country stable after the next general elections.

Mr. Temporary Deputy Speaker, Sir, there is a lot of illusion that it is the rungu that keeps the country intact. It is the goodwill of Kenyans and on that the topic that comes up very frequently nowadays--- I do not know why the hon. Members have forgotten about that. There was a document launched on 16th February, this year, entitled Economic Reforms for 1996/98. It is the policy framework paper. If we want to get the definition of what is a policy framework paper, I do not want to do it now. The Minister for Finance has a document entitled, Development Rethinking Brethrenhood in its death. It defines very well what is development. If you go through the policy framework paper, that was launched with funfair by His Excellency the Presidency from page 53 up to the end, it has several items entitled objectives and policies, strategies and measures and then timing. If you look at the timing of all those objectives, each one of them has its time expiring without a word about what the Government wants to do. The Ministry of Finance and Treasury in particular---

The Assistant Minister for Finance (Mr. Keah): On a point of order, Mr. Temporary Deputy Speaker, Sir. I am at a loss. I am trying to ply through my book to see which pages he is referring to and I cannot trace them. Could he repeat those pages again, please?

Mr. Maore: Mr. Temporary Deputy Speaker, Sir, I wish the hon. Assistant Minister would be more attentive on what we are saying. I am talking about this document which is entirely reflected in his Budget in

order for them to get money from Washington through the World Bank and IMF. If he cannot be attentive and get the context, then he is harassing hon. Members when they are contributing.

Mr. Temporary Deputy Speaker, Sir, if you look at the catalogue of the reforms which the Government has promised to undertake between 1996 and 1998, all the items that fall under for 1996 have passed without a word from Treasury as to when they intend to effect them. That is where I am getting my point. We are dealing with a Government that is very tall on promises, but very short on action. They will be able to promise Heaven when they see donors sitting around the table and say, "we are going to do this; we give the Opposition permits for rallies; we are ready for democracy; NSSF will be privatised and legislation is going to be brought---" All those from the catalogue, but none of those has been done. If we are dealing with the Government that is not even honest itself, that is why---

The Assistant Minister for Finance (Mr. Koech): On a point of order, Mr. Temporary Deputy Speaker, Sir. I do not wish to interrupt the hon. Member, but I think he is misleading the House and the nation because I have read that framework paper and quite a good number of things which have been recommended for reforms have been done. There are only a few which are waiting to be done and there are already some Bills in this House to effect those particular reforms. So, I think the hon. Member should not mislead the House.

Mr. Maore: Mr. Temporary Deputy Speaker, Sir, I did not want at all to refer to the issues, but for clarification purposes, to ensure that I am relevant with what I have said, I will just mention one issue here. There was this issue of National Cereals Board. In order to ensure that there was long term sustainability of the liberalised maize markets, it was supposed to be effected in March, 1996, but it has not been done so far.

Another one is on the environment. The Government was supposed to focus on the implementation of NEP in June, 1996, by coming up with a comprehensive sectoral environmental policy paper by June, 1996, but it has not done so.

As regards railways, the Government was supposed to restructure Kenya Railways so as to improve its efficiency. A policy paper on the restructuring Kenya Railways by the Government was supposed to be out before February, 1996, but has not been done.

As regards the Kenya Ports Authority, the Government was to complete the negotiations on the improvement of the port for the next 10 years by 31st March, 1996, but they have not completed even signing the contract; they are still in the process of negotiating so that some Government officers can get what they want.

There are several others, for example, on the energy sector, the Government was supposed to invite investments by March, 1996, but so far nothing has happened.

The point that I wanted to emphasise on is that you are dealing with the Government that will always be able to promise heaven when they know they are going to deliver hell. If you have to do these things voluntarily there is no World Bank, no International Monetary Fund (IMF) or anybody who draws a policy framework paper for anybody, it is the person who is under receivership who prepares the proposal on which to be bailed out after you have run yourself bankrupt.

Mr. Temporary Deputy Speaker, Sir, we do not want this propaganda that some sectors of the society are agents of foreign masters. If you want to know which of the two sides; that is that side and this side, uses donor money as its life support system it is the Government. If it is okay for them, it should be okay for everybody else.

Mr. Temporary Deputy Speaker, Sir, another issue that we need to raise is that of corruption. For a long time the Government has learnt one trick. It is the one of using scarecrows. The scarecrow is supposed to scare the people who are very vigilant about monitoring corruption. For a long time, and we noticed it last month or early this month when there was a debate on Kenya Co-operative Creameries (KCC), instead of the Government shouldering the responsibilities, there was massive propaganda from the Office of the President and from State House on Members of Parliament so that they can shift the gear from the Government to the Minister for Agriculture. It did not work. When there was massive corruption and looting of Central Bank through the Treasury, they wanted to shift all the gears and put them on the Minister for Finance. When there were problems relating to strikes in the universities in the 1980s and later on, they were saying it is the Minister for Education who was responsible for this unrest. The point that Kenyans need to be told clearly is that there is no single Minister who actually runs anything to do with the Ministry. If they attempt to run it, I want to say that ---

The Temporary Deputy Speaker (Mr. Wetangula): What do you want to say Mr. Maore? That is what you are talking about.

Mr. Maore: No, but if you have a Minister for Finance who is not responsible for how money was taken from the Treasury to go and construct Eldoret Airport without authorisation of one pound from this Parliament, then we are in problems. Three days ago we had a group of --

The Assistant Minister for Finance (Mr. Keah): My point of order is that the hon. Maore is misleading

this House by insinuating that the hon. Minister for Finance does not know where the monies that have been voted by this Parliament have gone to. Could he stop misleading the House?

Mr. Maore: Mr. Temporary Deputy Speaker, Sir, I am a member of the Public Accounts Committee. I am talking from an informed angle and not an emotional one. What I am stating here is that --- If you do not provoke me, I will not talk about the issues that are before the Public Accounts Committee. I am not interested in doing that. But, what I am stating is that a lot of the things the Ministry does --- You will hear that there are cases of no invoices, they do not know who went and negotiated and they bring in fake things. If you do not understand that this corruption can ruin your budget, then we are in trouble.

Mr. Temporary Deputy Speaker, Sir, the other issue that we need to emphasise on is that of irrational taxation on certain items that have a wider bearing or immense impact on the general economy. You hear a Government shouting from the roof tops on how they want to bring down inflation, speed up economic growth and the same Government in the same morning has increased petroleum products taxation. The petrol price at the pump is 56 per cent. Now, if you are the Minister for Energy who usually gets the taxation from Treasury, then the Permanent Secretary of Energy has turned out to be a trade unionist which is actually a testimony that the trade union movement has been compromised or has actually has been finished by the Government through complacent officials. The Permanent Secretary is the one who has been pressurising and complaining about the increases in petroleum products. If the Government is worried about inflation, the best way to bring down inflation is to reduce the amount of taxation on fuel or on petroleum products.

Mr. Temporary Deputy Speaker, Sir, sometimes in the past it was okay to keep on targeting petroleum because that was the only form of injecting hard cash because all other methods of taxation were full of loopholes. So, the easiest one was to go through the petroleum products. Now that we have Kenya Revenue Authority who are collecting an average of way above Kshs1 billion per day, we need to have the petroleum products taxation formula reviewed by the Treasury so that we can bring down the cost in the entire economy that has been messed up by the frequent increases in petroleum products taxation.

Mr. Temporary Deputy Speaker, Sir, on top of that, the Government in general is the one that needs the Finance Bill or the Appropriation Bill passed by this House. It is very important that the money we pass for each Ministry is used for the intended purposes. The issues of insecurity is making life for Kenyans a nightmare. Questions of insecurity are scaring away investors. They are scaring away the tourists. But, the most important aspect of this issue is that they are bringing in a very strong doubt and concern between the Kenya Government and its citizens for that is where there is a contract to govern. And the first assignment or the contract from the Government to its citizens is security of the lives of those citizens and their property.

Mr. Temporary Deputy Speaker, Sir, I am one of those people who are very, very sceptical that there can actually be people who can, sit, for example a group of 40, to organise and raid a village for three hours and there is not even a single suspect who can be able to unearth the mystery by giving information to a police force that is renown all over Africa as being very efficient as well as brutal and crude. They are not able to arrest people who can sit, organise, plan and execute robbery in several parts of the country. One of the commentaries in the Press refers to the frequent and rampant cattle rustling as a way of an illegal and unconstitutional redistribution of cattle. We all know the kilometres per hour that a cow can be able to cover. Now, if you have 300 or 1,000 cattle stolen, there is no way they can have an upward mobility unless they are transported fast. There is now way that they can move across the land and just evaporate. We have heard stories and tales that there is no will or there is complicity from the Government agents to perpetrate cattle rustling. We are going to have a large section of this country in economic trouble, which will result in insecurity because people who have lost their cattle may organize to raid their neighbours. It was stated here, by none other than a Minister of the Government that for the Government to pursue the Samburu cattle, the Samburus have to return the ones they took from Meru. I hope it was a slip of the tongue, and I hope it was not what he meant. It is not fair if we keep passing the Budget and keeping quiet about it. It is important to get concerned with the day-to-day management of revenue.

Mr. Nyagah: On a point of information, Mr. Temporary Deputy Speaker, Sir. The question of security has been talked about by very many people and we are getting very concerned. Every day when you read the newspapers, you see how many people have been murdered, how many people have been robbed of their personal belongings, animals, clothes, food and the rest.

The Temporary Deputy Speaker (Mr Wetangula): You are advancing an argument. Give him information!

Mr. Nyagah: I am giving him information! It has been alleged by many people that the question of insecurity has something to do with the Government. This is because, Embus have lived in peace for very many years; yet we are now being told by a man called Lee Njiru of the Presidential Press Service and who is very close to the President, that we must get rid of everybody else in Embu, and yet this is a man who works in State House.

He has even once removed a sword in public in presence of the PC and there was no action taken against him. The man has not even been summoned to record a statement. How can I not discuss about security with concern? In my own area, we have fights between the Kambas, Kikuyus, Embus and the Mbeeres because of statements emanating from Mr. Lee Njiru. So, that question of security must be addressed by this Government or lose the job.

Mr. Maore: Thank you for that addition.

The Temporary Deputy Speaker (Mr. Wetangula): You know very well that, that was not an addition. It was just an argument.

Mr. Maore: Mr. Temporary Deputy Speaker, Sir, another issue worth emphasising in the management of Government's revenue, is whereby we should allow the civil servants or the technocrats to run efficiently, key departments that are entrusted to them. There is a body called Kenya Revenue Authority. Whatever it has taxed---

The Assistant Minister for Lands and Settlement (Mr. Sumbeiywo): On a point of order, Mr. Temporary Deputy Speaker, Sir. It is becoming a bit difficult to follow the proceedings of the House when three hon. Members here; hon. Ntimama, hon. Orengo and hon. Koech are discussing their personal affairs and they are about to clash here. Could you ask them to discuss the matter in low tones?

Mr. Maore: Mr. Temporary Deputy Speaker, Sir, it is good to have vigilant policemen.

Mr. Orengo: On a point of order, Mr. Temporary Deputy Speaker, Sir. You just know what has been happening in KANU. I am trying to teach them how to bring KANU "A" and "B" together, without fighting and we were discussing very well.

The Assistant Minister for Finance (Mr. Keah): On a point of order, Mr. Temporary Deputy Speaker, Sir. Is the hon. Orengo in order to mislead this House and this nation that he is a teacher, teaching KANU and bringing KANU together? Is he in order to mislead this House when KANU is intact, it is one party and united in the whole country?

Mr. Achieng' Oneko: On a point of order, Mr. Temporary Deputy Speaker, Sir. I think Mr. Orengo was in order, because we asked him for consultations and we were not disturbed by the consultations he was carrying out with the hon. Minister who is my good friend.

The Assistant Minister for Finance (Mr. Koech): On a point of order, Mr. Temporary Deputy Speaker, Sir. Is hon. Orengo in order to claim that he is the best teacher, while he is graduating from a university which is disintegrating?

Mr. Maore: Mr. Temporary Deputy Speaker, Sir, I think Members are enjoying the debate. The issue of revenue collection, the procedures and the process must be strictly adhered to, for the Government to get its fair share of the revenue due to it.

*[The Temporary Deputy Speaker (Mr. Wetangula)
left the Chair]*

*The Temporary Deputy Speaker (Mr. Ndotto)
took the Chair]*

Mr. Temporary Deputy Speaker, Sir, between April and August this year, there has been quite some dance between the Treasury and Ministry of Transport and Communications over the Motor Transport Department. In April, Treasury directed the Motor Transport Department to be taken to Kenya Revenue Authority. It reached somewhere and somehow, some ill will did get into some officers either outside the Government or wherever it was and Treasury was coerced into returning the Motor Transport Department back to the Ministry of Transport and Communications. The purpose of getting it out of the Ministry at first was to ensure that the money collected which is quite a lot, is very well taken care of and finally ends up in the Consolidated Fund. The amount of corruption that goes on in Nyayo House does not require somebody to be an investigator to know it. You just need to walk in there and you notice everybody in a corrupt mood.

Mr. Temporary Deputy Speaker, Sir, we cannot understand why the Government which is so keen in looking for any cents they can lay their hands on, should take back the Motor Transport Department back to the Ministry of Transport and Communications, and yet, those loopholes have not been sealed. It is very well understood that there were attempts by some power brokers to ensure that when it is taken back to the Ministry of Transport and Communications, they would organize some deals and then this Department would be privatised and then, they would make some billions of Shillings.

Mr. Temporary Deputy Speaker, Sir, I would like to ask Treasury not to be running from one scandal to

